# KIZAZI KIPYA

KISEDET
Kigwe Social Economic Development and Training

## TASWIRA YA UTEKELEZWAJI WA MRADI: HUDUMA ZA USAIDIZI ZINAZOLENGA WATOTO WA MITAANI NA UKATILI DHIDI YA WATOTO KATIKA WILIYA YA DODOMA.

Kizazi Kipya ni mradi uliotekelezwa na kutiliwa nguvu na mashirika ya Asasi za kiraia za (KISEDET, IDYDC, CARTAS, BABA WATOTO, CHEKA SANA, AMANI, ARAMANO, ACC na IHAMBI) ambao walifanya kaza chini ya uongozi wa Railway Children Africa kutoa huduma za VVU. mradi ulitekelezwa katika wiliya 84 ikiwemo majiji 6 ya Tanzania ambayo ni Arusha, Dar-essalaam, Dodoma, Iringa, Mbeya na Mwanza ambapo huduma ya VVU ilipewa kipaumbele.

Taarifa hii imeandaliwa kulingana na kazi zinazofanywa na KISEDET kama mdau mmojawapo wa Kizazi Kipya, uliotekelezwa katika wilaya ya Dodoma chini ya ushirikiano wa (Railway Children Africa) walioandaa taratibu za kiutendaji na PACT Tanzania.
Utekelezwaji ulifanyika kupitia taarifa iliyotolewa na RCA kwa kuhudumia watoto wanaofanya kazi na kuishi mitaani mwaka 2018 kwa kushirikiana na KISEDET, Safina Street Network, Pact Tanzania, Ipsos na serikari ya Tanzania ndani ya kata 41 za manispaa ya Dodoma.

Tafiti zilionesha namba kubwa ya watoto na vijana walioko mitaani chini ya miaka 25 ikisimamia 501 ambao kati yao wavualana ni **376 (75%)** na wasichana pia ambao ni **125 (25%)**. Pamoja na udhalilishaji wa ngono na aina nyingine za unyanyasaji wa kimwili na kihisia kati ya watoto ni asilimia **(70%)**.

Mradi wa Kizazi Kipya ulikuwa ni wa miaka mitano (2017-2021) uliolenga kuondoa unyanyasaji dhidi ya watoto, kulinda na kuwajibika kata kata tano hasa zenye unyanyasaji wa watoto katika jiji la Dodoma-Kizota, Kikuyu, Chang'ombe, Mnadani na Makole. Mradi ulilenga makundi matatu (Familia, mtaani na vijana) kubaini changamoto za watoto wanaoishi mitaani pamoja na unyanyasaji wanaopitia.

Mbinu ya mtaani ililenga kuwatoa watoto umri wa miaka 1-14 kutoka mitaani kwenda kwenye familia salama au watu wa kuaminika: Mbinu ya familia ililenga familia za watoto walioko mitaani walioathiriwa na tabia za unyanyasaji kwa kutoa vipindi kwenye familia ili kuzuia unyanyasaji dhidi ya watoto: na mbinu ya vijana ililenga vijana wa mitaani (umri 15-18) waliathiriwa na dawa za kulevya na kuwaunganisha na sobber.

Tathimini ya mwisho wa mradi iliyofanyika (2021) ilionesha 92% tabia za unyanyasaji zilipungua majumbani baada ya wazazi kupatiwa mafunzo ya ACT-RSKP na idadi ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani imepungua kutoka 501 hadi 386. Tathimini pia ilionesha kuwa watoto 386 bado wanaishi na kufanya kazi mitaani; 160 wamekumbwa na ukatili wa namna mbalimbali hasa wa kingono kwa mabinti kati ya miak 15 – 18.

Aina hii ya watoto walijihusisha na biashara za usiku ambazo ziliwapa unyanyasaji wa kingono iliyopelekea mabinti 6 kupata maambukizi ya VVU/UKIMWI. Na hawakuweza kupatiwa msaada kutoka sehemu yoyote ile.

Watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani ni kipengele kilichoibuliwa na wizara ya Afya, maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto mwaka 2018, ikikadiriwa watoto waliopo mitaani kuwa ni 800,000. Hata hivyo tathimini iliyofanywa mwaka 2018 na RCA kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania, KISEDET Safina street network, Pact Tanzania na Ipsos, ilionesha kata 41 za jiji la Dodoma zilikuwa na watoto na vijana wa mitaani chini ya miaka 25 wakiwa 501 kati yao **376 (75%)** ni wavulana na **125 (25%)** ni wasichana. Sababu zilizowapelekea kuwa mitaani ni unyanyasaji wa kijinsia na umasikini.

Kuangalia mafanikio na uwiano uliobainishwa na RCA na KISEDET kwa pamoja juu ya mafanikio ya mradi wa Kizazi Kipya (2021-2023) ikiwa na lengo la kubaini unyanyasaji mmajumbani, ukatili wa kimwili na kihisia kwa watoto pamoja na umasikini zikiwa ni sababu zilizowatenganisha watoto na familia zao.

Utafiti ulionesha zaidi kuwa Dodoma ni ya tatu kati ya majiji sita yenye unyanyasaji kwa watoto na vijana walioko mitaani( 53% ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani walipata unynyasaji majumbani na maeneo ya wazi kama vile Nyerere squere, soko la majengo, mwanga baa, chako ni chako, na stendi ya mkoa, watoto na vijana hawa walikumbana na ukatili wa kingono, na aina nyingine za unyanyasaji wa kimwili na kihisia

## DESCRIZIONE DELL'INTERVENTO

Mradi wa Kizazi Kipya ilioanzishwa na Pact, RCA na KISEDET wa kuwasaidia na kuwaunganisha watoto na vijana chini ya miaka 25 wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Shughuli zilipangwa kulinganisha tathimini ya mwaka 2018 iliyobainisha kuwa aina hii ya watoto wamepata ukatili na kupata athali ya kimaisha kihisia, kimwili, afya na maendeleo ya kijamii, madhara ya kiafya na maendeleo ya kijamii.

Ili kutoa huduma kwa watoto wanaoishi mitaani; wadau wa kizazi kipya walinakili mbinu za utekelezwaji wake katika Nyanja tatu- za mitaani, familia na vijana. Mbinu hii ilichukuliwa kutoka kwenye muongozo wa mpango wa Tanzania wa kuzia ukatili wa watoto na wanawake (2017/18-2021/22).

Mbinu ya mitaani inahusisha ushiriki wa wadau pamoja na maafisa ustawi wa serikali ambao wana mamlaka ya kuwatunza na kuwalinda watoto kama ilivyoelekezwa kwenye sheria ya mtoto. Kupitia wadau hawa, maafisa ustawi hutoa kibali kwa KISEDET kuwaopoa na kuwasaidia watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani; na kuchukua hatua zaidi ya kuendelea na mpango wa kufuatilia familia zao wakati huo mtoto anaishi kwenye makao.

Makao yapo chini ya uongozi wa Mratibu ambaye kila mara huitisha kikao cha kujadili masuala ya kila mtoto mmoja baada ya mwingine na kumpangia mtu atakayeshughulikia sula la mtoto.

Mfanyakazi anajukumu la kusimamia maendeleo ya mtoto kwa kutumia miongozo ya kubaadili hali tabia ikiwa na lengo la kumuunganisha kwenye familia yake hatua kwa hatua (kufuatilia, kumpa mahitaji ya usafi, chakula, malazi, vipindi mbalimbali na kuwaandikisha shuleni) pamoja na kuwapatia ujuzi wa kimaisha.

Muongozo huo kwa sasa una mada ishirini na tatu. Zinazoelekeza dhana mbalimbali za kutathimini na utoaji huduma. Shughuli za KISEDET huanza na hatua ya uopoaji, ambapo wafanyakazi huenda mitaani na kufamiana na watoto kupitia mazungumzo ili kupata taarifa za mtoto ambazo huingizwa kwenye fomu za kila mtoto. Taarifa nyingine huchukuliwa kwa kuangali muonekano wa mtoto ambazo zimeandaliwa na KISEDET. Hatua za mtoto kuingizwa kwenye makao hufuatwa baada ya mtoto kukubali na afisa ustawi wa serikali huambiwa ili kutoa kibali. Jumla ya watoto **430** waliopolewa kutoka mitaani kwenda kwenye makao.

*Mbinu ya familia* ilitokana na mafunzo ya watu wazima na watoto katika program ya kuwakuza watoto salama (ACT-RSKP).

Mafunzo haya yanalenga kubadilisha tabia za ukatili na unyanyasaji kama vile kuwatukana, kuwapiga zinazotokea katika malezi. KISEDET ilitumia mafunzo haya kwa wazazi/walezi 131 kupitia mafunzo ya wiki 9. Mafunzo yanalenga kupunguza ukatili baina ya wazazi; kuboresha mawasiliano baina ya wazazi na watoto wao na ndugu wengine; kuboresha mahusiano katika familia; kudumisha undugu; kuboresha hali ya kipato; na kubaini mahitaji ya watoto ili kuzuia utoro mashuleni.

Mbinu ya vijana inawelenga vijana wenye umri kati ya 15-18 ambao husaidiwa aidha kwa kuwapeleka sober au makao ya kutwa yaliyotengenezwa na KISEDET. Wakiwa kwenye makao ya kutwa au sober hupatiwa ushauri nasaha ambao hulenga kuwasaidia vijana walioathiriwa na unyanyasaji wa kihisia, kimwili, kukataliwa, malezi duni na unyanyasaji wa majumbani. Sober hutoa mafunzo juu ya madawa ya kulevya, ujuzi mbalimbali, elimu ya jinsia na biashara ili kuwaandaa vijana wajitegemee.



## Jedwali 1: Mifumo na mbinu zinazotumiwa na KISEDET kutekeleza Mradi.

| ACT-RSKP | Rufaa na kuwaeka watoto katika makao | Usaidizi kwenye makao/ Soba |
|---|---|---|
| Mbinu ya ACT-RSKP inalenga kutoa ujuzi wa malazi kwa wazazi<br>katili kupitia mafunzo ambayo huchukua wiki 9 zenye mada 8. Mada zinafundishwa ni:<br>• Tambua tabia za watoto wako.<br>• Unyanyasaji kwa watoto.<br>• Kubaini na kuhimili hasira za wazazi.<br>• Kuelewa na kuwasaidia watoto wenye hasira.<br>• Watoto na mitandao ya kijamii.<br>• Aina za nidhamu na malezi.<br>• Nidhamu kwa tabia chanya.<br><br>Mafunzo hutolewa kwenye vikundi vyenye watu 20 jinsia tofauti. Kila wiki kwa masaa mawili. Vipindi mbalimbali vya watoto kujifunza (kucheza na midori, kupeana habari) hufanywa kwa watoot wenye umri 0 hadi 8 kwenye vyumba tofauti chini ya usimamizi wa wafanyakazi. | Rufaa hutolewa na afisa ustawi wa jamii kwa kutoa ruhusa ya mtoto kukaa kwenye makao kwa ajili ya kupatiwa msaada wa kisaikolojia. Vipindi vya ushauri hutolewa chini ya miongozo waliopewa wafanyakazi au mwanasaikolojia. Mwanasaikolojia atatoa mafunzo na kuwaeleimisha namna ya kuthibiti hisia zao kwa masaa mawili kwa kila wiki Watoto watakaoshiriki hufuatiliwa maedeleo yao kila wakati Kwa kila kipindi, masaa ya nyongeza hutumiwa kukusanya na kupitia maoni waliyoyatoa watoto. Mafunzo hayo hufuata makubaliano ya kimataifa ya haki za watoto ya mwaka (2009) Vipindi huendeshwa na watoto wakiwa na mwenyekiti na katibu ambapo hutoa maoni na uzoefu wa kipi kiboreshwe. Majukwaa ya watoto hulenga:<br>• Kuwapunguzia mawazo na kuwapa uwezo wa kuendana na mazingira mapya.<br>• Ufahamu kwa watoto. Kujikubari kama binadamu ambae pia hukosea na kustahili msamaha kwa mtu yeyote.<br>• Kusaidia watoto kuhimili hisia na uwezo wa kuwasiliana na wazazi na walezi na jamii pia.<br>• Kuwasaidia watoto kuwa na hamu ya kuonana na wazazi wao. | Mbinu hii huwasaidia vijana walioathiriwa na unyanyasaji walioupata dhidi ya wazazi, walezi na jamii. Vijana wanaopata mafunzo ya sober wanatarajiwa: ·<br>• Kuachana na ulevi wa aina yoyote ile.<br>• Kujihusisha na biashara ndogondogo kama vile ufugaji kuku, bustani, useremala, uchomeleaji au kujiunga na vyuo vya ufundi kupata ujuzi zaidi wa kimaisha.<br>• Kuwa na elimu ya kutosha juu ya jinsia, usawa na kuepuka unyanyasaji |

Kwa ujumla, utekelezwaji wa mradi ulijumuisha mbinu zilizoruhusu ushirikishwaji wa wadau, watu binafsi na mamlaka za serikali za mitaa kupitia njia mbalimbali kama vile mikutano, redio na runinga.

## MATOKEO

Mwaka 2021 tathimini ya mradi wa Kizazi Kipya ilifanyika na kuonesha mafanikio katika mbinu zote za mitaani, familia na vijana.
Uopoaji na ubadilisha tabia, vijana **430 (99%)** waliopokelewa na KISEDET waliimarisha mahusiano yao, walibadilika tabia na kurudis.

Vijana waliofika kwenye makao ya kutwa kwa miezi miwili hadi matatu, 44 walikubali kwenda soba kusaidiwa katika vituo vya Arusha na Dar es salaam. Na imeonesha mafanikio ambao 40 wameachana na madawa ya kulevya. KISEDET huzingatia hili kwa kuwapeleka vyuo vya ufundi ili waweze kujitegemea kwa baadae.


Wazazi **131** (127 wanawake; 4 wavulana) waliopota mafunzo ya ACT-RSKP wamekuwa na mawasiliano mazuri na tabia njema majumbani. Mbinu hii pia inatumiwa na katika malezi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania kama vile Mwanza,Arusha, Iringa, Mbeya na Dar es saalam.

## UTEKELEZWAJI MAFUNZO NA USHAHIDI


Cha kujifunza kutoka kwenye tathimini ya mwaka 2021 ya Kikazi Kipya, katika kutafuta suluhu ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani; RCA kwa kushirikiana na KISEDET walitengenza mpango wa miaka miwili (2021-2023) kuendeleza mradi wa kizazi kipya ikilenga kuwaunganisha watoto na kutoa watoto  huduma kwa walengwa 270 kwa Dodoma.

Shughuli zinalenga kuondoa unyanyasaji majumbani, unyanyasaji kimwili na kihisia kwa watoto na kusaidia familia masikini kwa kuwapatia mitaji ya kibiashara ili waweze kuondokana na umasikini 2021 – 2023 mbinu za mradi wa kizazi kipya umejikita katika mfumo wa mafunzo kwenye familia ambao haukuwepo. Mafunzo yanalenga kujenga mahusiano mazuri kati ya watoto ili kuzuia ynanyasaji.

Mbinu muhimu ilichukuliwa ni ufuatiliaji wa familia, uunganisha watoto na familia zao na kuwasaidia mahitaji ya shule wakiwa kwenye familia zao.
Kuendelea kuwafuatilia kwa kuwatembelea kila wiki ili kubaini viashairia vya unyanyasaji wa kimwili na kihisia na namna ya kuviondoa (matukio yanaonesha ukatili wa kimwili na kihisia kati ya wasichana ni 68% na wavulana ni 71%). Unyanyasaji wa kihisia unaathiri takribani robo ya wavulana na wasichana.



## MAFUNZO LENGWA



Kila mbinu na mfumo huleta mafunzo mapya na matokeo pia katika kuendeleza michakato ya ubadilishaji wa hali tabia kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, vijana na wazazi wenye tabia za ukatili.

Hata hivyo, kuwaweka watoto katika makazi salama, imekuwa salama kuliko mfumo mwingine wowote. Vipindi vya ushauri vinavyotolewa kweny makao vinasaidia kuhimilisha hisia na tabia za watoto. Kwa mfano, kabla ya kuwa kwenye makao watoto 430 (310Me na 120Ke) walilipotiwa kuwa wamefanyiwa ukatili wa aina mmbalimbali lakini baada ya kupatiwa vipindi tabia na hisia ziliimarika kwa 90%.
Hii imesaidia kuwaunganisha watoto na familia zao na shule. Vyuo kwa kupata mafunzo.

## MAREJEREO:


1. Street-connected children in Tanzania: Head Count Findings 2017/ 2018, Dar-es-salaam
2. NPA-VAWC in Tanzania: 2017/18 -2021/22, December 2016, Dar-es-salaam



This intervention profile was co-authored by KISEDET and Impact and Innovations Development Centre (IIDC) Citation: Reintegration, Response and Support services tackling street connected violence against children in Dodoma city (2022) by KISEDET, Dodoma Tanzania.



Kwa taarifa zaidi

KISEDET
Plot7 Block 53 Nduka Street, Area A Chamwino Dodoma P.O Box 379, Dodoma, Tanzania

+255 (0) 759 458 315
www.kisedet.org